

Ifanye haki

# SHERIA NA HAKI

*Kwa kila Mwananchi*



Iwe shauku

ISSN 0000 - 0000

Toleo Na. 001

Jarida la kila miezi mitatu

Novemba - Januari, 2009

MAONI

# maoni ya professor

# Bodi ya Mhariri

Mhariri Mkuu: Prof. Chris Peter Maina


Masaidizi Mhariri: Iss-haq I. Shariff

Mwenyekiti: Harusi M. Mpatani

## Wajumbe:

Safia M. Khamis  
Yussuf A. Hassan  
Makame M. Khamis  
Emanuel P. Chacha

## Ifanye Haki



Iwe shauku

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa:

Simu: +024 2233784

P.O.Box: 3360 Zanzibar

Fax: +024 2234495

E-mail: [zlsc@hudumazasheria.or.tz](mailto:zlsc@hudumazasheria.or.tz)

Website: [www.hudumazasheria.or.tz](http://www.hudumazasheria.or.tz)

# Tahariri

**KITUO cha Huduma za Sheria Zaznibar (ZLSC) Kimeazishwa rasmi mwaka 1992 hapa Zanzibar. Madhumuni makubwa ya kuanzishwa kituo hiki ni kutoa msaada wa kisheria kwa wasiojiweza, walemavu, wanawake, na watoto.**

**Aidha, Kituo huandaa semina na waarsha zinazohusiana na mambo ya sheria, Haki za Binadamu, Utawala Bora na kufanya tafiti za sheria kwa madhumuni ya kisaidia maendeleo ya Zanzibar na Tanzania kwa jumla.**

**Kituo kimesajiliwa kupitia Sheria za Zanzibar na hutoa huduma zake bila ya malipo. Vile vile, Kituo hakina uhusiano wa aina yoyote na chama chochote cha siasa, ndani au nje nchi. Hutekeleza kazi zake kwa mujibu wa utaratibu wake.**

**Katika miaka yote kumi na saba (1992 – 2009) ya uhai wake, Kituo kmefanikiwa kuanzisha mahusiano na Jumuiya mbali mbali za kisheria na kufanya kazi kwa mashirikano na mashirika ya Kimataifa kama vile Shirika la Umoja wa Mataifa na Maendeleo (UNDP).**

**Vile vile, Kituo kimeweza kuchapisha vitabu vy'a Sheria ikiwemo uchapishaji wa Ripoti ya Haki za Binadmu Zanzibar. Vitabu hivi vimesambazwa katika Maktaba mbali mbali ziliopo ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kusaidia sekta ya sheria.**

**Kwa viegezo vy'a aina yoyote, Kituo kmefanikiwa kutekeleza malengo kwa zaidi ya asilimia 70, jambo ambalo ni faraja na mfano wa kuigwa na Jumuiya nyengine zisizo za Serikali.**

**Katika hatua kuhakikisha kinawafikia wananchi kwa njia tofauti, Kituo kimeamua kuchapisha Gazeti lake ikiwa ni chombo maalum cha mawasiliano.**

**Gazeti hili tunaamini litasaidia kusambaza elimu ya sheria kwa ujumla.**

**Sera ya Gazeti hili itakuwa ni kuelimisha Umma. Gazeti litabeba habari na makala za Sheria zilizofanyiwa utafiti wa kina na kuandikwa na wataalamu wa sheria.**

**Makala zitakazochapishwa na Gazeti hili zitakuwa ni fupi fupi kwa sababu ya nafasi ya Gazeti lakini zitakidhi haja kwa wasomaji.**


*Maliyana*

**WANANCHI wote manombwa kusoma Gazeti hili la Kituo kwa madhumuni ya kujifunza zaidi na kupipma maendeleo ya utendaji kazi wa Kituo. Tunakaribisha barua za maoni kutoka kwa wasomaji na mchangi wa makala kwa ajili ya kuelimisha umma.**

**Aidha wote watakaopenda kuchangia au kutia maoni yao katika jarida la sheria na haki wanatakiwa wajitambulische kwa majina pamoja na anuani zao ili kuleta ufanisi, ukweli na uwazi katika kuendeleza Jarida hili.**

**Aidha wote watakaopenda kuchangia au kutia maoni yao katika jarida la sheria na haki wanatakiwa wajitambulische kwa majina pamoja na anuani zao ili kuleta ufanisi, ukweli na uwazi katika kuendeleza Jarida hili.**

# Z'bar yaadhimisha siku ya haki za binaadamu duniani



**T**ANGU kutolewa Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu mnamo tarehe 10 Disemba 1948 sasa ni miaka miaka sitini na moja (61), Mataifa mengi duniani yamekuwa yakiadhimisha kuzaliwa kwa tamko hilo kila ifikapo tarehe 10 Disemba. Kwa kuandaa mada na midahalo mbilia mbali mbali inayohusu Haki za Bindamu; pamoa na kutoa tamko rasmi kila mwaka Maadhimisho hayo yanapofanyika. Na kwa mwaka huu 2009 tamko rasmi la Umoja wa Mataifa lilitolewa siku ya Haki za Binadamu Duniani ni "Watu wote huzaliwa sawa na huru, kemea aina zote za udhalilishaji".

Zanzibar nayo iliadhimisha siku hiyo Kimataifa mnamo tarehe 10 Disemba 2009 kwa kuweka midahalo mbali mbali inayohusu haki za Binadamu ambapo kilele chake kiliazimishwa katika Ukumbi wa Bwawani Zanzibar na Mgeni Rasmi aliekuwa Rais wa Zanzibar Mh. Amani Abeid Karume.

Na kwa upande wa Pemba maadhimisho hayo yaliandaliwa na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar siku ya tarehe 10 Disemba 2009, ambapo yaliadhimishwa kimataifa kuanzia saa mbili na nusu asubuhi mpaka saa saba kamili mchana huko katika Ukumbi wa Chuo cha Ualimu cha

Benjamin W. Mkapa Wete Pemba. Maadhimisho hayo yalifungu-

liwa Rasmi Kimataifa na Mgeni Rasmi Afisa Mdhamsini Wizara ya Nchi Katiba na Utawala Bora Mh. Hemed Rashid, ambaye alipata nafasi ya kutoa nasaha zake kwa kulieleza kwa kifupi Tangazo la Umoja wa Kimataifa la Haki za Binadamu, pia amesema kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inathamini na kuzilinda emhaki za Binadamu na mwisho Mgeni Rasmi huyo alisema kuwa jukumu na wajibu wa kuheshimu haki za Binadamu sio tu la Serikali peke yake bali pia amewataka wananchi walioshiriki katika maadhimisha hayo, kuwa na wajibu wa kuzilinda haki hizo miongoni mwao.

Mbali na ufunguzi na nasaha hizo za Mgeni Rasmi pia Kituo cha Huduma za Sheria katika kutekeleza dira yake waliandaa mada mbali mbali zilizobeba dhamira Haki za Binadam, mada hizo ni pamoa na Haki za Binadamu katika katiba ya Zanzibar (1984) na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) na Haki za Binadamu, kuhusiana na Tamko la Umoja wa Mataifa. Mada hizo ziliandaliwa na kutolewa na Wajumbe wa Kituo cha Huduma za Sheria akiwemo Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo Mr. Iss-haq I. Sharif na Mjumbe kutoka Bodi ya mdhamin wa Kituo Mh. Safia M. Khamis kuititia mada hizo Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar waliandaa majadiliano na maoni kwa

wananchi walioshiriki katika maadhimo hayo, wananchi walio wengi walionekana kutoa maoni juu ya ukiukwaji na uvunjwaji mkubwa wa haki za binadamu katika jamii ya Zanzibar.

Kupitia maoni na mijadala huo Kituo cha Huduma za Sheria kimekiri kuwa upo uvunjwaji mkubwa wa haki za Binadamu hivyo kituo kimechukwa jukumu la kutoa mafunzo yanayohusu haki za binadamu kwa wananchi wote wan ngazi za utawala na ngazi za chini.

Wananchi walioshiriki katika maadhimisho hayo pia walionesha kilio chao cha ukosekanaji mkubwa wa haki za binadamu kuititia mashairi yaliyosomwa na kuandaliwa na wanafunzi wa Skuli ya Sekondari Kizimbani Wete, Pemba.

Maadhimisho hayo yalifungwa rasmi na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Huduma za Sheria Mr.Iss.-haq I. Shariff, ambapo aliyafunga rasmi maadhimisho hayo kwa kuwataka wananchi wawe na wajibu wa kufuatilia na kuzisoma kwa vitendo haki za binadamu zilizomo ndani ya Katiba ya Zanzibar (1984) na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977).

Mwisho kabisa maadhimisho hayo yalitumbuizwa na ngoma ya asili iitwayo "Msewe "iliyatayarishwa na wanafunzi wa Skuli ya Mchanga Mdogo Pemba.

# Zijuwe sheria za ardhi



**ARDHI** ni moja katika rasilimali muhimu hapa Zanzibar. Ardhi ina historia ndefu. Tunaweza kuigawa historia ya radhi katika vipindi viwili tofauti. Kipindi cha kwanza ni wakati Zanzibar ilipokuwa chini ya utawala wa wageni kutoka nje ya nchi.

Na kipindi cha pili ni baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Vipindi hivyo viwili vinatoa picha kamili ya historia na sheria za ardhi zilizopo kabla ya Mapinduzi na zile za baada ya Mapinduzi.

Hata hivyo, kwa madhumuni ya makala hii tutaangalia zaidi kuhusu sheria za ardhi zilizotungwa baada ya Mapinduzi. Na sheria zote hizi zimekuja ili kuweka mazingira mazuri ya kumiliki na matumizi ya ardhi kwa wazanzibari wote.

## MAANA YA ARDHI

Ardhi ni sehemu ya dunia yenye mkusanyiko wa mchanga na udongo. Kwa mtazamo wa sheria neno "ardhi" lina maana pana zaidi ya hiyo ya awali iliyoitajwa hapo juu.

Kwa mujibu wa kifungu cha 2 za Sheria ya Matumizi ya Ardhi ya 1992, ardhi inatafsiriwa kujumuisha ardhi yenyewe, pamoja na ile sehemu ya ardhi iliyoitajwa na maji pia na vitu vyote vinavyoota juu ya ardhi yakiwemo majengo na vitu vyengine vyote vilivyoshikana na ardhi isipokuwa miti iliyoainishwa wazi na inayomilikiwa tofauti na ardhi iliyo.

## SHERIA ZA ARDHI

Zipo sheria za ardhi zifuatazo:-

- (1) Sheria ya Kumiliki Ardhi No. 10/1990 Land Adjudication Act.
- (2) Sheria Ya Matumizi ya Ardhi No. 12/1992 Land Tenure Act.
- (3) Sheria Ya Mahakama Ya Ardhi No. 7/1994 Land Tribunal Act.
- (4) Sheria Ya Uhaulishaji Ardhi No 08/1994 Land Transfer Act.

## UMILIKAJI WA ARDHI

Kwa mujibu wa Sheria Ya Matumizi Ya Ardhi Nam. 12 ya 1992, Serikali ya Mapinduzi ya

Zanzibar ndio inayomiliki ardhi yote iliyopo Zanzibar. Mzanzibari ana haki ya kuhodhi na kutumia ardhi (Right of Occupancy). Haki ya kumiliki ardhi, kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha sheria hii iliyoitajwa hapa juu, haki ya matumizi ya ardhi inaweza kupatikana kupitia njia moja ya zifuatazo:-

- (a) Kupewa na Serikali; mtu anaweza kumiliki ardhi mara moja kwa ajili ya kilimo na mara mbili kwa ajili ya makaazi.
- (b) Kutambuliwa kwa haki ya matumizi ya ardhi kupitia maamuzi ya Mahakama ya Ardhi.
- (c) Kurithi.
- (d) Kununua.
- (e) Hiba.





## MASHARTI YA UMILIKI ARDHI








- (a) Kwa mzanzibari asiyepungua umri wa miaka 18.
- (b) Ardhi isajiliwe tokea mtu anapoipata.
- (c) Kuitumia ardhi hiyo kwa mujibu wa Serikali inavyotaka.
- (d) Kuiendeleza ndani ya miaka miwili.
- (e) Mtumiaji haezi kuigawa au kuipunguza ardhi hiyo.
- (f) Mtumiaji anaweza kutoa hiba au kuikodisha kwa masharti yaliyowekwa kisheria na kusajiliwa katika siku 60.
- (g) Mtumiaji anaweza kurithi kwa mujibu wa sheria.

## KUKATISHWA HAKI YA UMILIKI ARDHI

Serikali ambayo kisheria ndio mmiliki ardhi yote Zanzibar inaweza kumyanganya au kukatisha haki ya kuhodhi ardhi kutoka kwa mtu yoyote hata kama ikiwa amepewa kihalali isipokuwa kukatishwa huko kutakua kwa sababu zifuatazo:-

- (a) Kwa maslahi ya Taifa (kwa mujibu wa kifungu 56 cha Sheria hii). Serikali inaweza kuchukua ardhi ya mzanzibari kwa sababu za msingi na kwa manufaa ya wananchi kwa mfano: kupitisha njia, kujenga hospitali, sehemu za viwanda. Hata hivyo, masharti ya kuondoshwa kwa maslahi ya Taifa:- (i) Lazima ithibitishwe na Mahakama ya Ardhi (ii) Mwenye kuondoshwa alipwe fidia kwa thamani halisi ya vitu vyake vilivyomo katika ardhi yake.
- (b) Sio mzanzibari (kwa mujibu wa kifungu 57 cha Sheria hii) (i) Waziri anayehusika anaweza kumuondoshea haki hiyo wakati wowote.
- (c) Endapo mmiliki anajaribu kuhaulisha haki yake kwa asiyekua mzanzibari (kwa mujibu wa kifungu 57 (b)).
- (d) Endapo mmiliki ameshindwa kuitumia ardhi.





# Makarani wa mahakama wapatiwa mafunzo

**M**AFUNZO ya Marani wa Mahakama yalitayarishwa na Kituo cha huduma za sheria Zanzibar (ZLSC) kwa kushirikiana na Mahakama Kuu ya Zanzibar.

Mafunzo hayo yalifanyika kwa muda wa siku nne; siku mbili kwa upande wa Pemba na siku mbili kwa upande wa Unguja.

Kwa upande wa Pemba , mafunzo hayo yalifanyika siku ya tarehe 11 na 12 Disemba, 2009 katka Ukumbi wa Makonyo ,Wawi ,kuanzia saa 2:30 asubuhi hadi saa 9:00 mchana.

Kwa upande wa Unguja yalifanyika siku ya tarehe 19 na 20 Disemba , 2009 katika Ukumbi wa Skuli ya Elimu Mbadala hapo Rahaleo , saa 2:30 asubuhi mpaka saa 9:30 mchana.

Mafunzo hayo yaliwashirikisha Makarani wote wa Mahakama za Unguja na Pemba pamoja na wasaidizi wa sheria kutoka katika majimbo yote ya Unguja na Pemba.

Mara nyingi mafunzo haya hutolewa kwa dhamira ya kuwafanya washiriki kuweza kutambua haki na wajibu wao wa kazi katika kulinda na kukuza haki za binadamu ili kuleta mabadiliko katika mfumo mzima wa Mahakama.

Mafunzo hayo yalifunguliwa na mgeni rasmi Mheshimiwa Hemed Rashid ambaye ni Afisa Mdhamsini Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora, hii ni kwa upande wa Pemba. Na kwa upande Unguja yalifunguliwa na Mgeni Rasmi Mheshimiwa Jaji Mshibe Ali Bakar ambao wote kwa pamoja walitoto nasaha zao kwa Makarani wa Mahakama ikiwemo ile ya kuwatatak watunze maadili yao ya kazi wanapokuwa kazini.

Mada zilizowasilishwa katika mafunzo hayo ni kama zifuatazo:-

- Haki za Binadamu kama ili-vyoiezwa katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na ile Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mada hii iliwasilishwa na Mkurugenzi wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar, Ndugu Iss-haq I. Shariff.

- Haki za Binadamu na maendeleo ya jamii ambayo iliwasilishwa na Bi Safia Masoud Khamis . Yeye alizungumzia zaidi Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Kuanzia kifungu cha 11 hadi kifungu cha 25 (a) ambavyo vyote kwa pamoja vinachambua haki hizo zikiwemo haki ya kuishi na ile haki ya kumiliki mali.

- Utendaji na maadili ya shughuli za Mahakama . Mada ambayo iliwasilishwa na Mheshimiwa Yose Mlambwina ambaye alizungumzia maadili ya watumishi wa Umma na haki zao. Pia alizungum-

zia suala la wa Mahakama kwa kuzingatia Sheria No. 13 ya 1999,

inayojumuisha mipaka ya kazi karani wa Mahakama, suala la mavazi na usafi wa mwili pamoja na kuijendeze kitaaluma.

- Sheria ya ,mwenendo wa makosa ya Jinai Zanzibar, mada ambayo iliwasilishwa na Ramadhan A. Nassib kutoka Afisi ya Mkurugenzi wa mashataka wa Serikali (D.P.P). Mwasilishaji alizungumza mwenendo mzima wa kuwakamata wash-tumiwa , kuwahoji , kuwapakuwa pamoja na mwenendo wa mashtaka yenye ya-napofikishwa Mahakamani mpaka kufikia maamuza ya mwisho.

- Mwenendo wa Makosa ya .Madai Zanzibar mada hii iliwasilishwa na Dr. Hamud I. Majamba ambaye alielezea taratibu za Mahakama zikiwemo zikiwemo zile za kuandika Hati za madai na hati za majibu ya madai.

Pia alizungumzia suala zima la ku-suhulisha madai pale tu yanapofikishwa Mahakamani bila ya kuyafikisha kwenye vyombo husika.

Dr. Majamba litoa ushauri kwa Makarani wa Mahakama kuacha kufanya kazi za Sheria ambazo kisheria hawaruhusiwi kuzifanya wao zikiwemo zile za kuandika hati za madai na zile za majibu ya madai kwa wateja.

Baada ya mada hizo kuwasilishwa, Washiriki walipangwa kwa makudi na kupewa maswali ambapo kila kundi liliwasilishwa na mtu mmoja wa kusoma majibu hayo.

Vile vile kulikuwa na majadiliano na kupokea maoni kwa makunzi hao. Kituo cha Huduma za Sheria kimebaini mambo yaafuatayo:-

- i) Kwamba watumishi Watumishi (Makarani ) hao wa Mahakama hawakuwa na mwamko n a uelewa juu ya sheria za Watumishi wa Umm na , zikiwemo zile za

maadili na wajibu wa Makarani.

- ii) Walikuwa hamwafahamu wajibu wao wa kazi kwani walikuwa wakiandika baadhi ya mambo ambayo kisheria hawarushiwi, Mfano kuandika hati za Madai.

- iii) Makarani walio wengi walikuwa hawafahamu suala zima la haki za Binadamu zilizomo ndaniya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na ile ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977.

- iv) Makarani walio wengi hawana elimu juu ya sheria ikiwemo uhuru wa Mahakama, Utawala wa sheria na uendeshaji wa kesi za Madai na zile za Jinai.

Hivyo basi, baada ya kupata mafunzo hayo walihidi kujirekebisha na kufanya kazi kwa mujibu wa sheria za watumishi wa Umma.

Tarajio la kituo cha Huduma za sheria Zanzibar (ZLSC) ni kuendesha na kutoa elimu ya sheria mara kwa mara kwa Makarani waMahakama ili waweze kufahamu wajibu na maadili ya kazi zao katika kuhakikisha suala la utekelezaji wa haki za Binadamu linafanikiwa.

Hivyo basi Wadau wa sheria na Asasi za Serikali hazina budi kushirikiana kwa pamoja kiliflikia lengo hili.

S emina hii inafungwa na Mheshimiwa Hemed Rashid, Afisa Mdhamsini Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora kwa upande wa Pemba. Na Unguja imefungwa na Mheshimiwa Khamis Ramadhan Abdalla, Mrajis Mahakama Kuu Zanzibar.

Wafungaji hawa kwa pamoja walitoto nasaha zao kwa Makarani zikiwemo zile za kutekeleza majukumu yao na kuzingatia yale yote ambayo wameyapata katika mafunzo hayo ili wawe mfano mzuri wa kuigwa na kusifiwa katika jamii ambayo inajali na kulinda haki za binadamu.

# Mafunzo ya vyama vya wafanyakazi

**J**AMII iliyelimika ni mihimili imara katika maendeleo endelevu. Hii ni kwa sababu kwamba jamii hiyo hufanya mambo yote kwa kufuata utaratibu maalum uliofutiliwa na kutekeleza majikimi yake kwa umakini.

Hata hivyo jamii na makundi mbali mbali hayawezi kufikia hapo kama michago ya taasisi tofauti haijawekwa kuwapatia taaluma husika kwa mujibu wa shughuli za kundi hilo.

Mafunzo kwa vyama vya wafanyakazi ni moja ya hatua za msingi zinazochukuliwa ili kufikia ..... yaliyoelezwa hapo juu. Mafunzo haya ni muhimu katika uwepo wa utumishi ulio bora na wenyewe ufanisi katika sehemu tofauti za kazi. Hii ni kwenye vyama vya wafanyakazi vinakusanya makundi tofauti ya watumishi katika sekta mbali mbali ziwe zile za Umma na za binafsi. Hatua hii ..... Kwenda sababu na ule msemo usemao "Ukimuelimisha mwanamke umeelimisha jamii nzima." Hivyo mimi na imani yangu kuwa "ukielimisha vyama vya wafanyakazi umeelimisha yote ya wafanyakazi."

N I dhahir kwamba mafunzo ya vyama vya wafanyakazi mbali ya kuvizwisha vyama hivyo kufahamu zaidi mchango wake katika utumishi na kwa wanachama wao huvinidisha vyama hivyo sehemu ya wafanyakazi haki na wajibu wao katika kazi.

Taaluma inayohusu haki, wajibu na majuku ya wafanyakazi, na wafanyakazi ni vyombo muhimu

Sana na ikitolewa ipasavyo ni sababu ya mabadiliko ya mazingira katika sehemu za kazi na itapelekea utendaji bora.

Kwa lengo la kufanikisha azma hiyo, ndio ilikuwa msukumo uliosababisha Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar [ZLSC] kuandaa na kuendesha mafunzo kwa watendaji wa vyama vyama vya

Wafanyakazi Zanzibar kati ya terehe..... Unguja na Tarehe..... Pemba.



Mafunzo haya hayakuendeshwa kwa bahati mbaya bali yalitokana na mifumo yenye na pia yalilenga katika utekelezaji wa hoja ya ..... ya kituo ya kutoa elimu ya kisheria kwa jamii kwa mantiki ya kuongeza uelewa juu ya haki na wajibu wao.

Jumala ya sheria 6 zinazohusu ajira zilifanaliwa, ..... na kujadiliwa nawawezeshaji na washiriki zikiwemo:

- i) Sheria ya Ajira
- ii) Sheria ya mahusiano kazi

Kwa upande wa washiriki Kituo kwa kushirikiana na shirikisho la vyama vya wafanyakazi ZATUC Kilikusa

nya jumla ya washiriki 70 {35 Unguja na 35 Pemba} kutoka vyama tofauti vya wafanyakazi katika mafunzo hayo.



Jambo la kusikitisha ambalo libainika ni kuwa hata mionganoni mwa washiriki hao walikuwa mionganoni mwao walikuwa tayari ni waathirika wa matatizo tofauti katika sehemu zao za kazi kama vile kunyimwa haki ya likizo kutohaka na kutfahamu taratibu za kisheria na haki yao hiyo kwa waajiri na waajiriwa.

Mbali na hayo Kituo kilibainikuwa jamii

iko tayari kujifunza nakupokea aina tofauti za taaluma.

Mwisho ni imani yetu kuwa mafunzo haya ..... na elimu iliyotolewa ..... kulinda na kupata haki zote majukumu.

**H**AKI ya dhamana sio msamiati mpya kwa wananchi. Mara kwa mara, msamiati huu hutanganzwa na vyombo vya habari pale kunapokuwepo kesi ya jinai mahakamani. Dhamana ni haki ya katiba. Lakini mahakama ina mamlaka kumpa au kumnyima mshtakiwa.

Uamuzi wa mahakama kumpa au kumnyima mshtakiwa hutegemea na mazingira ya kesi na mshtakiwa kutimiza masharti ya dhamana. Baadhi ya wakati, masharti ya dhamana huwa ya kawaida na baadhi ya wakati huwa magumu na mshtakiwa hushindwa kuyatimiza.

Haki ya dhamana ni mionganini mwa haki za msingi za binaadamu. Ni haki ya mtu kuwa huru. Asili ya haki za binaadamu hazitokani na katiba wala mikataba ya kimataifa. Ni haki za binaadamu wote kutokana na nasabu ya wao kuwa binaadamu.

#### NINI HAKI YA DHAMANA?

Haki ya dhamana ni haki ya mtu kuwa huru wakati anakabiliwa na tuhuma au shtaka la kuvunja sheria. Hapa ndipo tunapokabiliwa na suala zima la kupima kati ya kulinda uhuru wa mtu au kikundi cha watu bila ya kuathiri uhuru wa watu wengine ambao pengine kwa kupewa uhuru mtu mmooja au kikundi cha watu bila ya kuhatarisha uhuru wa watu walio wengi katika jamii husika.

Sheria ya Uendeshaji Mashtaka ya Jinai (Criminal Procedure Act No. 7 of 2007) ina vipengele kuanzia kifungu 150 mpaka kifungu 161 vinatoa maelezo juu ya haki ya dhamana. Kwa kweli, haki ya dhamana ni utaratibu ambao uhuru wa mtu ambao unahitaji kurudishwa katika hali ya kawaida kwa masharti au bila ya masharti yatayowekwa na Mahakama yenyewe mamlaka ya kesi husika.

#### NINI NAFASI YA MTU ALIYEPEWA DHAMANA?

Mtu yeoyote anayekabiliwa na shtaka anahesabiwa kuwa ni mtu huru mpaka pale kosa lake litakapothibiti na mahakama kumtia hatiani kutokana na vifungu vya sheria. Kesi inaweza kuchukua muda mrefu, hata zaidi ya miaka miwili, bila ya kumalizika.

Pindipo uhuru wa mtu huyo husika utaachwa kuwa mashakani au hatarini kwa kipindi chote hicho, itakuwa sawa na kumvunjia pamoja na kumnyanganya haki yake ya kuwa kiumbe huru kama zielezayo katiba zetu.

Aidha, tafsiri ya haki ya dhamana inaweza kuelezwaa kuwa ni kitendo cha kumuachilia mtu ambae alikuwa anashikiliwa au amewekwa mahabusu au hali ya kizuizi fulani kwa kutoa au kuweka dhamana au ahadi kwa madhumuni ya kumrudisha kwa wahusika siku atakayohitajika.

#### HAKI YA DHAMANA HUMPA MSHTAKIWA UHURU WA MOJA KWA MOJA?

Lazima ielewewe kwamba haki ya dhamani sio haki ya mshtakiwa kuwa huru moja kwa moja. Ni haki ya kuwa nije ya ulinzi wa kushikiliwa na vyombo vya dola. Na badala yake, mshtakiwa anakuwa chini ya dhamana ya wadhamini ambao hutoa ahadi ya kumrudisha mahakamani siku na tarehe atakapohitajika.

# Ijuwe haki ya dhamana

Dhamani sio uthibitisho ya uhuru kamili. Wakati mwengine dhamana hutolewa kwa masharti ambayo mdhaminiwa akiyavunja haki hiyo ya dhamana huondolewa na Mahakama.

#### KATIBA ZINASEMA NINI KUHUSU HAKI YA DHAMANA?

Ibara ya 12 (1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 na Ibara ya 11 (1) na (2) and Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kwa pamoja zinaleza kwamba "binaadamu wote huzaliwa huru, na wote ni sawa," na "kila mtu anatahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake."

Mshtakiwa anahesabiwa kuwa huru mpaka pale mahakama itakapomtia mahakamani kwa kosa aliloshtakiwa nalo. Mshtaki ana wajibu wa kuthibitisha kosa dhidi ya mshtakiwa katika kigezo cha "pasi na mashaka yoyote."

Kabla ya mshtaki hajathibitisha kosa la mshtakiwa, mshtakiwa ana haki kuwa mtu asie na hatia. Na kwa mantiki hiyo, mshtakiwa ni lazima atendewe sawa na mtu yoyote ambae hana hatia. Ibara ya 12 (6) (b) ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 inaeleza kwamba "mtu anaeshtakiwa kwa kosa la jinai hatatendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo."

Mshtaka yapi hayana dhamana?

Mshtaka ya yafuatayo mshtakiwa hapaswi kupewa dhamana (1) Kuua kwa makusudi

(2) uhaini (3) wizi wa kutumia silaha (4) kupatikana na silaha za moto na (5) usafirishaji wa madawa ya kulevyaa.. mashtaka mengine yote yaliyobaki haki ya dhamana inatolewa.

#### NANI MWENYE MAMILAKA YA KUTOA DHAMANA?

Pamoja na kuwa dhamana ni haki ya msingi lakini bado inabaki katika mapendekezo au matakwa ya Jaji au Hakimu. Hata hivyo, inasisitizwa kwamba, jaji au hakimu lazima atoe maamuzi ya haki ya dhamana kutokana na hali halisi ya kesi na sio maamuzi yanayotokana na utashi wake binafsi.

Katika kesi ya Republic V/S MT.12153 L/CPL WAGENYI (1983) TLR 141, shahidi wa kesi hiyo aliswekwa rumande na mshtakiwa kufutiwa dhamana yake na Hakimu wa Wilaya kwa sababu eti alikuwa ananukia harufu ya pombe.

Katika rufaa ambayo ilisikilizwa na Jaji Mfalila alisema sehemu ya maneno yafuatayo " watu wanaopewa madaraka wayatumie kwa uangalifu na wasihusise mambo yao binafsi katika kutoa uamuzi, hii itasababisha matokeo yasiyo halali kama ilivyo katika kesi hii."

# Siku ya msaada wa kisheria

**S**IKAU ya Msaada wa Kisheria ni siku ambayo msaada wa Kisheria hutolewa bure kwa watu wasio na uwezo na uelewa wa kisheria,pamoja na wale waliokuwa hawana uwezo wa kuweka wakili au mtu wa kuwasimamia mahakamani.

Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984,imeeleza haki mbalimbali za kibinaadamu ambazo kila mwananchi anatakiwa azipate Kisheria ,mionganini mwa haki hizo ni haki ya kupata Usawa mbele y asheria kama ilivyoelezwa katika ibara ya 12 (1) ya katiba ya Zanzibar, ibara hiyo inasomeka kama;

“Watu wote ni sawa mbele ya sheria , na wanayo haki, bila ya ubaguzi wowote,kulindwa  
Na kupata haki sawa mbele ya sheria”

Ili kuhakikisha haki hiyo inafanikiwa kila ifikapo tarehe 13 disemba ya kila mwaka nchi nyingi zimekuwa zikiadhishwa siku ya Msaada wa Kisheria , ambapo watu wote upata haki yao ya kimsingi ya kupata msaada wa kisheria .Siku hii huadhimishwa Kitaifa toka ilipoasisiwa Kimataifa .N a lengo kuu la siku hii ni kusaidia wanyonge,maskini,na wasiojiweza ili kupata haki zao.

Adhimio la siku ya Msaada wa Kisheria huadhimishwa Kila ifikapo tarehe 13 Disemba ya kila mwaka Kituo cha Msaada wa kisheria , katika kutekeleza majukumu yake kwa kuheshimu Sheria za Zanzibar kinatoa , Msaada wa Kisheria ikiwa ni pamoja na kutoa msaada wa kupata wakili au msaidizi wa sheria katika kusimamia mwenendo mzima wa kesi katika Mahakama,msaada huu wa kupatiwa wakili bila ya malipo unatolewa kwa watu maskini na wasiojiweza kama ilivyoelezwa katika mwenendo wa kesi za madai oxxxvii, r II (I) (2), (3) kwa kuthibitika na kuomba mahakamani kwa Mfunguaji kesi hiyo ni maskini.

Maadhimisho ya siku hiyo ,Kituo kilishirikiana na jumuiya ya wanasheria wanawake Zanzibar (ZAFELA), Zanzibar law society(ZLS), Wafanyakazi wa ofisi ya DPP, Pamoja wafanyakazi wa Mahakamani, katika maadhimisho hayo walitoa ushauri na misaada mbali mbli ya kisheria.

Kwa mwaka huu Msaada wa Kisheria ulifanyika huko Gombani,Wilaya ya Chake Pemba. Msaada huo ulianza


kutolewa kuanzia saa 2.30 asubuhi hadi saa 8 mchana.  
ZLSC kikishirikiana na ZLSC,ZAFELA,DPP's office na Mahakama kiliendesha misaada ya

Kisheria na kupata kesi 11, ambapo kesi zamadai zilikuwa 2 kesi ya vipande vya kupigia kura ilikuwa ni 1.

Ifanye haki

# SHERIA NA HAKI

*Kwa kila Mwananchi*



ISSN 0000 - 0000

Toleo Na. 001

Jarida la kila miezi mitatu

Novemba - Januari, 2009